



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

MAELEKEZO YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024

Kwa mujibu wa Kanuni Na.8 (1)(2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Viongozi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya, Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa anatoa maelekezo kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 2024 kama ifuatavyo;

Tarehe ya Uchaguzi:

Kwa mujibu wa Tangazo la uchaguzi lililotolewa kwa kuzingatia kanuni ya 4 ya Kanuni za uchaguzi wa viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (Tangazo la Serikali Na. 571, 572, 573 na 574), uchaguzi utafanyika **tarehe 27 Novemba 2024.**

(a) Muda na sehemu ya kuandikisha wapiga kura:

Kwa mujibu wa Kanuni ya 11 (GN. Na. 571/Mamlaka za Wilaya, zoezi la uandikishaji wa wapiga kura litafanyika kuanzia tarehe 11 hadi 20 Oktoba 2024 katika vituo vilivyopangwa

(b) Muda na mahali pa kufanyia uchaguzi:

Kwa mujibu wa kanuni ya 31 GN Na. 571, Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, mwenyekiti wa kitongoji na wajumbe wa halmashauri ya Kijiji utafanyika kwenye vitongoji na vituo vingine vilivoelekezwa katika vijiji husika.

(c) Wito kwa Wakazi wenye sifa za kupiga kura:

Kwa mujibu wa kanuni ya 13 GN. Na. 571, wakazi wote wenye umri wa miaka 18 au zaidi na waliokidhi masharti ya kisheria wanahimizwa kushiriki katika uchaguzi huu.

(d)Wito kwa wagombea:

Kwa mujibu wa kanuni ya 15 GN. Na. 571, wakazi wenye umri wa miaka 21 au zaidi wanaotaka kugombea nafasi za uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji wanahimizwa kuchukua fomu za kugombea katika Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(e) Kuchukua na kurudisha fomu:

Kwa mujibu wa kanuni ya 17 GN. Na. 571, fomu za kugombea zitatolewa na kutakiwa kurudishwa **kuanzia tarehe 01 hadi 07 Novemba 2024** kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(f) Uteuzi wa wagombea:

Kwa mujibu wa kanuni ya 18 GN Na. 571, Uteuzi wa wagombea utafanyika tarehe 08 Novemba 2024.

(g)Pingamizi dhidi ya uteuzi:

Kwa mujibu wa kanuni ya 23 GN. Na. 571, muda wa kuweka pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea ni kuanzia **tarehe 08 hadi 09 Novemba 2024** na uamuzi wa pingamizi utatolewa kuanzia **tarehe 08 hadi 10 Novemba 2024**.

(h)Rufaa dhidi ya uamuzi kuhusu pingamizi la uteuzi:

Hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 23 (3) GN. Na. 571, rufaa zitapokelewa kuanzia tarehe 10 na 13 Novemba 2024 na uamuzi wa kamati ya rufaa utatolewa kuanzia **tarehe 10 na 13 Novemba 2024**.

(i) Kampeni za uchaguzi:

Kwa mujibu wa kanuni ya 27 GN. Na. 571, Kampeni za uchaguzi zitaanza **tarehe 20 hadi tarehe 26 Novemba 2024**. Kampeni hizi zitafanyika kuanzia **saa 2 kamili asubuhi hadi saa 12 kamili jioni**.

Ninatoa wito kwa wananchi wote wenye sifa kushiriki kikamilifu katika mchakato huu wa uchaguzi, kuanzia hatua ya kujiandikisha kwenye

orodha ya wapiga kura. Kujiandikisha katika orodha ya wapiga kura ni hatua muhimu inayompa kila mwananchi mwenye sifa haki ya kisheria kushiriki uchaguzi kama mpiga kura au mgombea. Hivyo, Wananchi wanahimizwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha ili kutumia haki yao ya kupiga kura au kugombea nafasi za uongozi.

Nafasi zitakazogombewa katika uchaguzi huu ni uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji. Hivyo, wananchi wenye sifa wanahimizwa kuchukua na kurudisha fomu za kugombea nafasi hizo kwa tarehe zilizoainishwa katika maelekezo haya. Ushiriki wa wananchi wengi katika kugombea nafasi hizi ni muhimu katika kukuza demokrasia na kuhakikisha upatikanaji wa viongozi bora kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mwisho, niwahamasishe Wananchi wa **Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa** kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi ambayo ni **Jumatano ya tarehe 27 Novemba 2024**, ili kuchagua viongozi bora watakaoongoza.

Imetolewa na:



MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA KONGWA

TAREHE: 26 SEPTEMBER, 2024

